

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika Barua za Shaaban Robert. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

### **Uchanganuzi wa Mandhari katika Barua za Shaaban Robert**

<sup>1</sup>Judith Kidigu Mwavali; <sup>2</sup>Dkt. George Obara Nyandoro & <sup>3</sup>Dkt. Owen McOnyango

<sup>1</sup>Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu Cha Kisii. Barua Pepe: [Mwajudi@gmail.com](mailto:Mwajudi@gmail.com)

<sup>2</sup>Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu Cha Kisii. Barua Pepe: [Nyadgeorge@yahoo.com](mailto:Nyadgeorge@yahoo.com)

<sup>3</sup>Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi, Chuo Kikuu Cha Kisii, Barua Pepe: [Omconyango@yahoo.com](mailto:Omconyango@yahoo.com)

#### **Ikisiri**

Makala hii inachanganua mandhari katika Barua za Shaaban Robert. Hoja kuu ni kwamba licha ya mandhari kuwa na umuhimu mkubwa kisanaa, kipengele hiki hakijachunguzwa na kuchanganuliwa ipasavyo katika fasihi ya Kiswahili. Ingawa Shaaban Robert ameutumia ufundi huu kwa ufanisi mkubwa katika barua alizomwandikia nduguye Yusuf Ulenge, suala hili bado halijapewa umuhimu unaostahiki. Msingi wa makala ni kwamba Barua za Shaaban Robert ni mtungo ambao haujachanganuliwa na utanzu wa barua katika fasihi ya Kiswahili unastahili kutiliwa maanani. Mandhari ni muhimu katika kuzielewa na kuzihakiki barua za Shaaban Robert na utanzu wa barua kwa jumla. Mandhari zilizochanganuliwa ni za aina tatu kuu: mandhari ya wakati; mandhari ya mahali na mandhari ya kihistoria. Shaaban Robert amesuka mandhari kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii kupitia Ulenge. Mandhari imetumika kuchora wahusika pamoja na kuwasilisha maana ya mwandishi kwa hadhira inayowakilishwa na Ulenge. Maudhui yanayojitokeza katika barua za Shaaban Robert kwa Ulenge yanahusu elimu. Ujumbe wa mwandishi ni kuhimiza vijana kutilia maanani suala la elimu kama msingi mkuu wa ukombozi na kujitegemea. Barua za Shaaban Robert ni hazina ya fani na maudhui na mfano mzuri wa utanzu wa barua katika Kiswahili. Pana haja kubwa kutafiti kwa kina maana na matumizi ya mandhari katika Barua za Shaaban Robert pamoja na tungo nyingine za mwandishi huyu. Isitoshe, ni muhimu kwa uchunguzi kufanywa kuhusu ukuaji wa utanzu wa barua. Isitoshe, pana haja ya kuchunguza na kuhakiki matumizi ya barua kama mbinu ya kisanaa katika fasihi ya Kiswahili. Mwelekeo huo mpya utadhihirisha umaarufu na mchango wa Shaaban Robert katika fasihi ya Kiswahili na kuonesha namna fasihi hii inavyodhihirisha sifa kuu kiutunzi na kimataifa. (Maneno 263)

**Maneno Makuu:** Mandhari; Barua za Shaaban Robert; Utanzu wa barua; Fasihi ya Kiswahili; Sanaa ya utunzi.

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

## **Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert***

<sup>1</sup>Judith Kidigu Mwavali; <sup>2</sup>Dkt. George Obara Nyandoro & <sup>3</sup>Dkt. Owen McOnyango

### **Utangulizi**

Makala hii inahusu uchanganuzi wa mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. Mwandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili Shaaban Robert ametumia mandhari kwa ufundi pevu wa kisanii katika barua alizomwandikia mdogo wake Yusuf Ulenge. Lengo la makala ni kuchunguza na kuchanganua jinsi ambavyo Shaaban Robert alivyoitumia mandhari kama kipengele cha utunzi ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii. Makala hii inahoji kwamba Shaaban Robert ametumia mandhari katika utanzu wa barua ili kuwasiliana na ndugu yake mdogo Yusuf Ulenge, vijana walioko shuleni na jamii nzima ya Waswahili.

### **Barua za Shaaban Robert**

Utanzu wa barua ni mpya katika fasihi ya Kiswahili. *Barua za Shaaban Robert* ni mfano mzuri wa utanzu huu mpya. *Barua za Shaaban Robert* ni mkusanyiko wa barua mbalimbali ambazo Shaaban Robert aliandika na kumtumia mdogo wake Yusuf Ulenge. Kitabu hiki kinasheheni barua mbalimbali zilizokusanywa na kuhaririwa na Mugyabusso Mulokozi na kuchapishwa mwaka 2002 miaka 40 baada ya kifo cha mwandishi.

Mtungo huu wa *Barua za Shaaban Robert* ni hazina ya fasihi ya Kiswahili. Fani na maudhui yaliyomo ni ya kiwango kilichopevuka mno. Shaaban Robert ametumia ufundi mkubwa kueleza ujumbe wa aina mbalimbali kwa jamii tofautitofauti. Ni kutokana na matumizi pevu ya fani ambapo mwandishi huyu amesifika sana katika faishi ya Kiswahili.

Shaaban Robert ni mtunzi mwenye ushawishi mkubwa sana katika historia na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Mulokozi (1991) Shaaban Robert ameithiri jamii kwa namna kubwa sana kupitia tungo zake. Mpaka sasa, tungo za Shaaban Robert zinazofahamika na zilizochapishwa ni 24. Idadi kubwa ya tungo zake, pamoja na ufundi wa hali ya juu uliotumika na maana ya kazi zake ni miongoni mwa sababu ambazo zimempa hadhi kubwa. Chatbar (2006) anasema kwamba licha ya Shaaban Robert kuaga miaka mingi iliyopita, mwandishi huyu bado yu ‘hai’ miongoni mwa walimu, wanafunzi na wahakiki wa Kiswahili kupitia tungo zake ambazo zinasomwa, zinafundishwa na kuhakikiwa katika viwango mbalimbali vya elimu, ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu. Ni kutokana sifa hizi ambapo makala hii inachunguza na kuchanganua mandhari katika *Barua za Shaaban Robert* kwa lengo la kutaka kuelewa kwa kina matumizi ya kipengele hicho kufanikisha mawasiliano na ujumbe.

Kwa mujibu wa Elistratov (1996), barua ina historia ndefu inayotokana na maendeleo katika jamii. Mtaalam huyu alizichunguza barua za awali zilizoandikwa na kuwasilisha kwa njia ya posta; tofauti na barua za kisasa ambazo zimeathiriwa na teknolojia ya habari na mawasiliano. Kwa upande wake, Cook (1996) anahoji kuwa baadhi ya wahakiki wa fasihi wa awali walidai kuwa barua haingeweza kuchukuliwa kuwa fasihi. Hata hivyo, mtaalam huyu amechunguza mtindo, historia, falsafa na matumizi ya barua na kutambua kwamba zinatekeleza majukumu ya kifasihi. Maoni ya Cook yanakubaliana na utafiti uliofanywa na Halsband (1958) uliodhihirisha

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

kwamba barua ina sifa zote za fasihi bunifu. Halsband aligundua kwamba mwandishi maarufu wa fasihi ya Kiingereza Samuel Johnson alipendelea sana kutumia mtindo wa barua. Hoja kuu ya Cook (1996) na Halsband (1958) ni kwamba ingawa kimsingi barua ni mawasiliano ya siri baina ya watu wawili, pale maandishi hayo yanapowekwa wazi na kuchunguzwa, basi yanapata sifa ya uhakiki ambao ni msingi mkuu katika fasihi ya aina yoyote. Ni kutokana na hatua za kihakiki na za kiutafiti ambapo barua zimepata sifa ya kuwa fasihi.

Kama ilivyo kwa historia ya barua, utanzu wa barua nao una historia ndefu ambayo inaonekana katika mabadiliko kwenye mtindo, maudhui na maana. Katika karne ya ishirini, barua zilionekana katika riwaya kama vile za Nabokov (*Lolita*, 1955), Doris Lessing (*The Golden Notebook*, 1962), Alice Walker (*The Color Purple*, 1982) na watunzi wengineo.

Barua inadaiwa kuwa muhimu sana katika fasihi andishi ya mwanadamu kwa kuwa ndio ulikuwa msingi na mwanzo wa riwaya. Kwa mfano, katika karne za kumi na saba na kumi na nane, barua zilikusanywa na kuunda riwaya ya kibarua ya Samuel Richardson iliyoitwa *Pamela*. Ruth Perry katika *Women, Letters and the Novel* (1980) anonyesha historia ndefu ya barua na uhusiano wake na riwaya. Nao Cook (1996) na Holman (1972) wanaeleza kuwa mikusanyiko mingine ya barua ilijenga msingi wa riwaya za awali za fasihi ya Kiingereza. Kwa mujibu wa Hutcheon (1982), matumizi ya barua katika riwaya ni ishara ya uhusiano baina ya fasihi na maisha ya mwanadamu.

Kuwapo kwa barua katika riwaya kuna maana kwamba utanzu wa barua ni muhimu na unastahili kuchunguzwa na kuhakikiwa. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa kuna tofauti kubwa baina ya barua za awali na zile za kisasa. Vivyo hivyo, kuna tofauti baina ya barua za kifasihi za awali na zile za kisasa. Miongoni mwa tofauti hizo ni umbo na muundo wake. Mandhari ni sifa ya kiumbo na kimuundo. Mandhari huchorwa na kutumiwa kama mbinu ya kifasihi. Hivyo basi, pana haja ya kuelewa maana na matumizi ya kipengele hiki cha fasihi.

Isitoshe, mwandishi wa barua anabadilika na kuwa mtunzi, naye mpokeaji anakuwa ni hadhira. Kwa wale wanaopata fursa ya kuzisoma barua zenyewe, nao wana wajibu wa kuwa wahakiki. Hivyo, barua inabadilika na kuwa fasihi inapokuwa na sifa hizo mbalimbali. Na kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi, barua zina sifa za kimuundo, kiumbo, kimaana, kimaudhui na kimatumizi. Masuala haya yenye umuhimu mkubwa kwa historia na maendeleo ya barua yanahitaji uchunguzi, maelezo na hata ufundishaji.

Hamu miongoni mwa watafiti na wahakiki kuhusu barua kama utanzu inatokana na ugunduzi unaotokea katika fasihi na uhuishaji wake. Haya ni kwa mujibu wa Altman (1982) anayeamini kwamba uchunguzi wa kipengele cha barua ni sehemu ya ukuaji wa maisha ya mwandamu pamoja na mabadiliko katika mifumo na sanaa zake ikiwa ni pamoja na fasihi. Naye Cook anasema kwamba binadamu anajisahili na kutaka kujielewa vyema zaidi, na hivyo kutafuta ushahidi kutoka kokote kule unakoweza kupatikana. Barua ni mawasiliano ya kisiri na wakati huohuo ya umma, hivyo ni msingi muafaka wa kuilewa jamii na maendeleo yake. Mandishi ya kale, kama vile barua, ni msingi mzuri wa kuelewa jamii. Barua hueleza hisia za mwandishi na jamii yake.

Ni katika muktadha huu makala hii inachunguza mandhari katika *Barua za Shaaban Robert* ili kuonesha namna ambavyo fasihi ya Kiswahili nayo ina sifa za kimataifa za utunzi. Zaidi ya hilo, kuna hofu miongoni mwa watafiti kwamba utanzu wa barua unafifia katika fasihi

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

kutokana na athari za kiteknolojia. Hii ni sababu nyingine ya utafiti wa *Barua za Shaaban Robert* ili kudhihirisha kwamba utanzu huu unaanza kuchipuka katika fasihi ya Kiswahili. Hapana shaka kwamba utanzu wa barua katika fasihi ya Kiswahili utapata msukumo na kukua.

Barua ambazo Shaaban Robert alimwandikia Yusuf Ulenge zimekusanywa, zimechapishwa na sasa zinafanyiwa uhakiki kama fasihi ya Kiswahili. Hatua ya kukusanya barua na kuzichapisha kama alivyofanya Mulokozi ni jambo ambalo lina historia kwingineko duniani. Uamuzi wa Mulokozi ni hatua muhimu sana katika uchunguzi wa barua katika Kiswahili kwa jumla na kwa uhakiki wa utanzu wa barua katika fasihi ya Kiswahili. Juhudu zinahitajika kuhakikisha kwamba ‘barua’ katika Kiswahili zinachunguzwa na kuhakikiwa. Na muhimu zaidi ni kuchunguza utanzu wa barua katika fasihi ya Kiswahili.

Umuhimu wa *Barua za Shaaban Robert* unadhihirika kupitia mtindo, maudhui na maana ya barua mbalimbali zilizomo kwenye mtungo huu. Ingawa Shaaban Robert alimwandikia mdogo wake, dhamira na lengo lilikuwa ni kwa vijana wa Uswahilini na jamii pana kwa ujumla. Kama ilivyo kwa tungo zake nyingine, Shaaban Robert ametumia jukwaa la barua kutujulisha masuala ya maisha, utu na hatima ya mwanadamu. Kwa kuzisoma barua alizomwandikia Ulenge, tunapata fununu kuhusu maisha ya Shaaban Robert tangu kuzaliwa Januari 1909 katika mji wa Tanga, wakati huo nchini Tanganyika, hadi kifo chake Juni, 1962. Kwa kipindi cha miaka 53 Shaaban Robert aliyafanya mengi kama mwandishi, mtumishi wa umma, mpiganiaji wa uhuru wa Tanganyika, na mwanaharakati wa kuiendeleza lugha na fasihi ya Kiswahili. Ni maisha haya ambayo Shaaban Robert ameyasimulia katika tungo zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na *Barua za Shaaban Robert*. Mtungo huu ni hazina kubwa katika fasihi ya Kiswahili.

*Barua za Shaaban Robert* ni mkusanyiko wa barua sitini na tisa ambazo Shaaban Robert alimwandikia Ulenge katika vipindi mbalimbali akiwa kwenye mandhari tofautitofauti alikofanya kazi. Ujumbe kwa mdogo wake ni umuhimu wa elimu na haja ya kufanya bidii masomoni. Mbali na elimu, *Barua za Shaaban Robert* zinatoa wosia kwa vijana kuhusu maadili, haki, uhusiano, matumaini, imani na dini na mapenzi. Huu ni ujumbe wenye umuhimu mkubwa kwa vijana wanapokabiliana na changamoto za maisha.

Mwandishi vilevile anasisitiza haja ya kuheshimu na kulinda utamaduni kama msingi wa maendeleo ya kijamii. Anaonyesha namna ambavyo lugha ya Kiswahili ni kipengele muhimu cha utamaduni wa mwafrica. Kiswahili kinaelezwa kuwa chombo na raslimali ya kuijenga jamii. Kwa vijana wa Afrika, utamaduni wao ndio ngao yao. Kiswahili kinatarajiwa kuwasaidia vijana kujielewa na kujieleza katika jamii zao.

Kitabu hiki vilevile kinachangia kueleza na kuonyesha safari ya maisha yake. Na kama ilivyo kwa safari nyinginezo, *Barua za Shaaban Robert* kina mandhari ya wakati na mahali mbalimbali.

### **Mandhari kama kipengele cha utunzi.**

Fasihi hujengwa kwa sifa kuu kadha wa kadha ikiwemo matumizi pevu ya kipengele cha mandhari. Kipengele hiki ni sehemu muhimu katika uandishi wa fasihi na huwa jumla ya mambo yanayojenga matukio katika fasihi. Matukio katika fasihi huwahusu wahusika wanaotenda

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

mambo kutokana na sababu fulani na yenye athari. Hivyo basi, mandhari ni kipengele cha sanaa ambacho hutumiwa na mwandishi wa fasihi ili kumsaidia kuisuka na kuiwasilisha kazi yake.

Mandhari ni dhana pana ambayo imefafanuliwa na kutumiwa na wataalamu mbalimbali kwa njia tofauti tofauti. Dhana ya mandhari huhusishwa na matukio ya kihistoria, kiutamaduni, kiwakati pamoja na maelezo ya kijiografia ambamo hadithi au maelezo hutokea.

Donna (1992) anaeleza mandhari kuwa ni uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi kwa kuwa humwezesha msanii kujenga hisia husika miongoni mwa wasomaji kwa kuyahusisha maelezo na mazingira husika. Anayahusisha mandhari na wahusika, mada pamoja na mtindo uliotumika katika kazi yoyote ile ya kisanaa. Hivyo basi mandhari hujitokeza kama dhana muhimu elekezi ambayo huwezesha ujenzi wa wahusika na utangamano wao kijamii.

Ntarangwi (2004) anasema kwamba ili kazi yoyote ya fasihi ieleweke na iwe ya kuvutia, haina budi kuwa na nguzo au msingi inamokulia. Kwa vile kazi ya fasihi huwa inamulika uhalisia wa aina fulani, basi bila shaka lazima iwe na ulimwengu wake. Tutaipima kazi ya fasihi kulingana na vile ilivyombwa.

Aghalabu mandhari huwa kigezo muhimu cha kuelewa au kueleza kazi ya fasihi. Jinsi mtunzi anavyojenga mandhari yake ni jambo muhimu katika kazi ya fasihi na huwa inamulika na kusaidia katika kuelekeza msomaji katika kuelewa zaidi kazi hiyo. Kwa kawaida, mandhari huwa ni sura ya mahali, hususan jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Mtunzi anaweza kutumia mandhari kueleza mazingira halisi ya kisa anachokisimulia katika kazi yake. Mathalan mtunzi anaweza kutuchorea mandhari ya pwani kwa kushughulikia vitu kama vile upwa wa ziwa, minazi na pia nyumba za makuti. Jambo hili huleta hali ya ufasaha katika utunzi wowote ule.

Kwa mfano, ikiwa mtunzi atasawiri mhusika maskini hohehahe katika maelezo yake, basi twataraji mahali anapoishi, jinsi anavyochorwa kimaisha na taswira yake kwa jumla iwe ya kudhihirisha hali halisi na ya kuaminika. Mandhari hivyo basi ni kipengele ambacho hutufichulia ni wapi na ni lini tukio fulani lilitokea.

Hivyo basi, mandhari ni mahala au pahali ambapo kazi ya fasihi hutokea. Mandhari hujumuisha vipengele vya wakati na mazingira ambamo wanajamii hutangamana. Vipengele vya wakati, mahali na mazingira ni muhimu katika ujenzi wa mandhari. Kipengele cha wakati haswa humwelekeza msomaji kuelewa nyakati palipotokea matukio na mazingira husika kama vile hali ya kitamaduni na ya kisiasa baina ya wanajamii. Kwa mfano, maelezo ya matukio kimandhari baina ya nchi iliyokomaa kisiasa huwa tofauti sana na yale katika nchi zilizokumbwa na vita. Vilevile, maelezo ya kiutamaduni kiwakati hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Pia, mandhari kiwakati hudhihirishwa na mabadiliko ya hali ya anga kama vile msimu wa kiangazi au masika.

Wamitila (2002) anaeleza mandhari kuwa ni mahali ama wakati tukio la kifasihi hubuniwa na kutendeka. Mandhari hufanikisha ujenzi wa hisia za msomaji au msikilizaji ama mtazamaji kwa misingi ya kazi ya fasihi inayowasilishwa. Mandhari pia ni sehemu ambapo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itatendeka. Kazi ya fasihi iwayo ile lazima iendane na sehemu au mahali ambapo matukio hutokea. Mandhari hutumika kurejelea wakati na sehemu ambamo matukio ya msuko hutokea. Hivyo basi mandhari ni kipengele muhimu cha fani katika

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

uchambuzi wa kazi yoyote ile ya fasihi na huweza kuonyesha uhusiano baina ya vipengele vingine husika katika kazi ya utunzi.

Masinde (2012) katika uchanganuzi wa maendeleo na mabadiliko ya maudhui katika ushahi wa Kiswahili anadai kuwa mazingira ya msanii pamoja na tajriba zake katika maisha huathiri kwa kiasi kikubwa namna anavyouona na kuusawiri ulimwengu na mtazamo wake humwelekeza anapotoa mapendekezo yake kuhusu jamii. Anaeleza mandhari kuwa kipengele muhimu katika kazi ya fasihi. Kipengele hiki huweza kukamilishana na vipengele vingine katika kazi ya fasihi ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Anazidi kueleza kuwa maana ya kifasihi inaweza kutazamwa kwa kuchunguza mazingira ya msomaji, mwandishi au kazi yoyote ile ya fasihi. Hii ina maana kuwa muktadha wa tamko au andiko fulani huathiri kwa kiasi kikubwa namna tamko au andiko linavyofasiliwa na msomaji au msikilizaji. Hivyo basi, kadri mazingira yake ya kibinafsi na kijamii yanavyoendelea kubadilika ndivyo tajriba yake inavyobadilika. Mabadiliko haya yanaweza kuelezwa kwa kuzingatia muktadha wa kihistoria.

Gakuo (1996) naye ameangazia swala la fani na uelewekaji wa *Utenzi wa Vita vya Uhuru* uliotungwa na Shaaban Robert (1945). Katika utafiti huu, Gakuo ameeleza kuwa ni muktadha wa kihistoria ndio uliomhamasisha Shaaban Robert kutunga utenzi huo. Anasema kuwa muktadha na mazingira yanayomzunguka mwandishi ikiwa ni pamoja na historia yake ndiyo hutumika kama mihimili na chemichemi ya mawasiliano na maudhui katika kazi yoyote ile ya kifasihi.

Kwa jumla, mandhari ni sehemu au mahali ambapo matukio ya hadithi au masimulizi au kazi yoyote ile ya kifasihi hutokea. Mahali penyewe huchukuana na kipengele cha wakati. Pia mandhari yanaweza kufasiriwa kama usawiri wa mazingira ambapo mahusiano na matukio baina ya wahusika huendelezwa. Kwa hivyo, mandhari huweza kujibu swali: Kisa au tukio lilitokea lini na wapi.

Mandhari pia huweza kuwa halisi au ya kufikirika. Mandhari halisi hudhihirishwa na vipengele kama vile baharini, njiani, msituni, kijijini na mijini ilhali yale yakufikirika hudhihirishwa na vipengele kama vile kuzimu, mbinguni na peponi ambavyo huwa ni dhahania tu. Mandhari haya huweza kusaidia katika uendelezaji wa maudhui kutokana na vile yanavyochorwa.

### ***Mandhari katika Barua za Shaaban Robert***

Mandhari hutokea kwa namna mbili kuu: kiwakati na kimahali. Mandhari ya kiwakati hudokeza ni lini jambo fulani lilitokea: Wakati huweza kuwa kipindi kama vile dakika, saa, siku, wiki, mwezi, mwaka na karne. Wakati unaweza kuwa mchana au usiku. Kuna pia mandhari ya kihistoria ambayo inasheheni wakati na mahali.

Katika *Barua za Shaabani Robert*, mandhari ya kiwakati imetokea kwenye barua kadhaa. Kwa mfano:

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika Barua za Shaaban Robert. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

Mf.1. **Barua Na.4** (uk. 30).

Moshi,  
Julai 4, 1931

Yusuf Ulenge,

*Barua yako nimesoma. Yote ulionieleza nimefahamu lakini majibu hasa ya barua yako nitaleta Jumaa-tatu. Nafikiri labda utaweza kufika Tanga ukiniahidi kuwa utarudi tena chuoni.*

*Nitaleta barua kwanza kwa bwana Mwalimu pamoja na gharama ya chuo kwa miezi mitatu – hapo ndipo nitakapokuletea majibu yangu yote.*

*Kwa heri!*

*Mimi nikupendae sana!*

S. Robert

Katika mfano huu, kuna mandhari ya wakati ambayo inajitokeza katika vipindi maalum:

Kwanza, mwandishi Shaaban Robert kwa mdogo wake Ulenge. Ulikuwa ni mwezi wa Julai.

Pili, mwandishi pia amebainisha tarehe maalum ya barua kuandikwa: nayo ni tarehe 4 mwezi huo wa Julai.

Tatu, mwandishi ameonyesha mwaka ambao ulikuwa 1931.

Wakati mwingine ambao mwandishi pia ameuonyesha ni siku ya Jumaa-tatu ambapo anasema angeipeleka barua kwa Ulenge.

Vilevile, kuna mandhari ya kipindi maalum. Mwandishi anazungumzia gharama ya chuo ‘kwa miezi mitatu’. Inavyoonekana, Shaaban Robert anarejelea kipindi maalum ambacho kinaelekea kuwa muhula wa masomo chuoni.

Isitoshe, mwandishi anagusia wakati ujao ambao matukio mawili yatafanyika: Jambo la kwanza ni pale Ulenge atakapofika Tanga. Tukio la pili ni pale atakapompelekea Ulenge majibu yake yote.

Katika mfano huu, mandhari ya wakati inadhihirika kwa aina sita: Mwezi; tarehe; mwaka, siku; miezi mitatu na wakati ujao wa matukio mawili.

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika Barua za Shaaban Robert. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

Mf.2. Barua Na. 13 (uk. 52)

HM. Customs,  
Moshi,  
4<sup>th</sup> September, 1932

Dear Yusuf Ulenge,

Kwa muda mrefu hujaniandikia. Sema! Neno ninalotaka kukuarifu leo ni hili: Nimekwoshalipa kwa Bwana Mwalimu wa Moshi Shs. 20/00; yaani, masurufu ya School kama desturi. Stakabadhi nimepata N. E69112 ya tarehe 3 September, 1932. Kwa hivi tafadhali mara iishapo livu yako fika kwa Bwana Mwalimu wa Tanga. Yeye, ninalotumaini kwamba atakupa warrant urudi School tena. Yumkini, lakini sina hakika, Bwana Chando, amekwisha mwandikia Bwana Mwalimu wa Tanga juu ya habari hii. Lakini iwapo ipo shaka kidogo, muombe Bwana Mwalimu wa Tanga asome waraka huu.

Tanga urudi upesi. Wanafunzi si vema kuchelewa. Wambie baba na mama salam zatoka kwa Roberts.

Wasaalam,

Shaaban Roberts.

Katika huu mfano wa pili, kuna mandhari ya wakati kama ifuatavyo:

<b>Tarehe</b>	4 <sup>th</sup> na 3
<b>Mwezi</b>	September
<b>Mwaka</b>	1932
<b>Kipindi</b>	‘Kwa muda mrefu...’
<b>Siku</b>	Leo
<b>Wakati</b>	‘...mara iishapo livu...’; ‘...urudi school tena’; ‘...amekwisha mwandikia...’; ‘...urudi upesi

Kwa upande mwingine, mandhari ya kimahali huelezea ni wapi tukio hutokea. Kila kisa katika fasihi huwa na sehemu au maonesho tofauti na kila onesho huwa na mandhari tofauti. Mahali pa upekee panaweza kutumiwa kutunga chanzo au asili ya mgogoro mpya. Katika upana wake, mandhari ya mahali yanaweza yakachukua dunia, nchi, jiji, mji, kijiji, kitongoji na hata ndani ya nyumba. Mazingira huimarisha kuelewa maisha ya wahusika na athari ya mazingira hayo katika mielekeo na falsafa zao. Kwa mfano, namna maisha ya Shaaban Robert kama mtumishi wa umma aliyefanya kazi katika Shirika la Posta yalivyouathiri uhusiano wake na nduguye Yusuf Ulenge. Maana halisi ya barua inaweza kupatikana tu pale ambapo uhakiki ni mpana na unazingatia muktadha mpana wa mahali na wakati na siyo tu yale yanayojitokeza kwenye maandishi yaliyoko kwenye ukurasa.



**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

Mf.3. **Barua Na.47** (uk. 122).

*HM. Customs,  
Longido,  
P.O Arusha,  
26 Machi, 1938*

*Dear Yusuf Ulenge,  
Mpwapwa.*

*Barua yako imewasili salama, na mimi natoa asante nyingi sana. Ningefurahi sana kujua mahali unapotazamia kutumia mapumziko yako safari hii.*

*Kweli sikukuambia ya kuwa kaka yako Jaffer alifika Dar es Salaam wakati nilipokuwa huko mimi na mama mdogo. Basi ijapo bwana huyu alifika mjini mapema sana, hakufika nyumbani kumtazama mama ambaye sisi wote atupasa mpaka siku ya pili. Vizuri sana!*

*Wakati nilipokuwa Dar es Salaam niliazimu kujenga; hata nimewahi kununua zaidi ya meta thelathini za mawe lakini tena ilitokea safari hii na mambo yote yamesimama. Nimemnunulia Miss Mwanjaa kijishamba kwa Shs. 400/- hivi.*

*Wasaalam,*

*S. Roberts.*

Katika barua hii, Shaaban Robert amerejela mandhari ya mahali kwa namna mbalimbali:

Kuna ‘HM. Customs’ ambayo ni ofisi ya Mkuu wa Forodha. Shaaban Robert alikuwa akifanya kazi katika ofisi hiyo.

Hiyo ofisi ya forodha ilikuwa sehemu ya Longido, barabara ya kutoka Arusha keulekea Namanga mpaka wa sasa wa Tanzania na Kenya. Kwa hivyo, Longido ni mahali maalum palipotajwa na mwandishi.

Ofisi ya forodha ya Longido inapatikana katika Mkoa wa Arusha ambao nao umetajwa na mwandishi kama mahali maalum.

Barua hii Shaaban Robert anamwandikia Yusuf Ulenge amabaye yuko shuleni Mpwapwa.

Shaaban Robert pia anarejelea mji wa Dar-es-Salaam katika barua yake.

Vilevile Shaaban Robert anataja ‘nyumbani’ na ‘kijishamba’ kama mandhari za mahali.

Mandhari ya kihistoria huelezea kipindi tukio linapojitokeza. Ni kipindi, au mwaka au mwezi gani? Katika *Barua za Shaaban Robert* mandhari ya kihistoria yanadhihirika kupitia wakati maalum wa siku, miezi, miaka na hata karne. Shaaban Robert alifanya kazi wakati wa kipindi cha uokloni na wakati huohuo ambapo Yusuf Ulenge naye alikuwa shuleni. Kipindi cha

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

ukoloni kilikuwa chini ya utawala wa Wazungu. Waafrika walifanya kazi katika mazingira mbalimbali. Matarajio yalikuwa mengi kuhusu namna ya kuvaa, kula, kuishi n ahata kuongea. Katika barua kwa nduguye Ulenge, Shaaban Robert mara kwa mara anawataja walimu kwa heshima. Kwa mfano katika Barua Na. 13 hapo juu, Shaaban Robert anaeleza: ‘Bwana Mwalimu wa Moshi’ na ‘Bwana Mwalimu wa Tanga’. Yumkini hawa walikuwa walimu wazungu.

Isitoshe, kwa kiasi kikubwa katika *Barua za Shaaban Robert* kuna mchanganyiko wa mandhari ya wakati, mahali na kipindi. Hali hii inadhihirika katika mifano ya barua zilizokuliwa hapo juu. Kuna tarehe, siku, miezi na miaka mbalimbali. Pia, kuna mahali kama vile miji ya Moshi, Tanga, Arusha na Dar-es-Salaam; vituo kama vile Longido; shule kuel Mpwapwa; nyumbani n ahata shambani. Hii ni mifano tu ya mandhari ya mchanganyiko.

Kwa ujumla, mandhari yaliyojitokeza katika *Barua za Shaaban Robert* ni ya aina tatu kuu: wakati, mahali na kipindi cha kihistoria. Mandhari hizi mara nyingi zimetokea kwa pamoja. Mandhari zina umuhimu mkubwa sana katika kazi hii ya Shaaban Robert.

### **Umuhimu wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert***

Mandhari ni kigezo muhimu kwa mhakiki katika kupima kueleweka kwa mtungo anaoushughulikia. Kwa kuzingatia mandhari ya kazi anayoihakiki, mhakiki huweza kufaidika katika kujibu maswali kadha wa kadha kama vile: Je, mtunzi ametuchorea mandhari yanayochukuana na wahusika pamoja na maudhui yake? Je, mandhari yanatekeleza jukumu gani katika kuelewa kazi nzima?

Ntarangwi (2004) anasema kwamba, wakati mwingine ni muhimu kutambua mazingira alimotungia kazi mtunzi kama njia ya kumsaidia mhakiki kuelewa zaidi sababu ya uchaguzi wa lugha na maudhui katika kazi husika. Hii ni kwa sababu mazingira anamotungia kazi huathiri sana uchaguzi wake wa lugha na jinsi anavyoendeleza maudhui yake. Kuyaelewa mazingira haya humsaidia mhakiki kutambua kinagaubaga maana ya mtunzi kutumia fani mbalimbali za lugha, kuweza kutambua kama palikuwa na mshawasha wa namna fulani uliomfanya mtunzi kuandika hivi na sio vile na pengine kutambua ni kwa nini kaandika kazi husika ya kifasihi. Kwa jumla ni jambo la ziada na muhimu kwa mhakiki kuyaelewa mazingira alimotungia kazi mtunzi ili kuelewa zaidi kazi ile.

Katika *Barua za Shaaban Robert* mandhari yanasaidia kuelewa maana hasa ya mwandishi hasa kupitia uteuzi na matumizi ya lugha pamoja na maudhui. Mazingira yalikuwa na athari kubwa kwa utunzi wa Shaaban Robert, hasa tukizingatia kwamba aliandika wakati wa ukoloni. Suala la elimu limejitokeza kuwa lenye umuhimu mkubwa katika barua za Shaaban Robert. Alimtaka Ulenge atilie maanani elimu kama silaha ya ukombozi na raslimali ya baadaye maishani.

Vilevile ni muhimu kwa mhakiki kuelewa kipindi au hali ya kihistoria alimotungia mtunzi kazi yoyote ile ya kifasihi. Jambo hili humwezesha mhakiki kutambua uhalisia wa maudhui na vilevile kuyaelewa zaidi maudhui hayo. Mabadiliko ya binadamu kiutamaduni kwa miaka mingi na mwendo wa jamii kiwakati na kinafsi ni mambo muhimu sana kwa mwandishi yoyote kwasababu mengi ya yale yaliyotendeka wakati uliopita katika historia huwa yanafungamana na mtizamo au picha ya yaliyopo na yajayo.

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

Mtazamo wa mambo ambayo huenda yakamkumba binadamu katika maisha ya baadaye huwa yanajikita kwenye misingi ya tajriba yake ya yaliyopita. Kinachojitokeza hapa ni kuwa, kazi nyingi mashuhuri za fasihi huathiriwa sana na historia pamoja na matukio yake. Kila kazi ya fasihi huwa na muktadha wa kiwakati, yaani muktadha ambao huainishwa kwa kurejelea kipindi fulani cha historia. Kueleweka kwake huchukuana na kuelewa kwa anayeisoma kipindi cha kihistoria kazi hiyo ilipotungwa. Waandishi katika kipindi fulani huwa wakati mwingine wanazingatia maswala sawa kwa kuwa na maadili sawa. Kufahamu kipindi alimotungia mtunzi huenda ikawa kigezo cha kumwezesha hata msomaji kutambua ni nini cha kutarajia katika kazi husika ya fasihi.

Shaaban amedhihirisha kuwa historia ina athari kubwa kwa mwandishi. Aidha, tajriba ya Shaaban Robert inajitokeza pale anapomsihi Ulenge kutilia maanani elimu ilia pate kuishi maisha mazuri baadaye.

Mahali patokeapo hadithi ni muhimu katika kazi yoyote ile ya kisanaa na huchangia pakubwa katika kuelewa mandhari husika. Mandhari haya huchangia pakubwa katika ujenzi wa wahusika na uendelezaji wa maelezo na dhamira ya mwandishi. Ni kutokana na maelezo ya mandhari ndipo msomaji huweza kutambua mkondo wa hadithi au matukio halisi. Jambo hili limehihirika katika barua za Shaaban Robert haswa anapowarejelea watu mbalimbali katika ukoo wake, pamoja na walimu wa Ulenge.

Mandhari vilevile humwelekeza msomaji kutafakari na kufahamu hali halisi ya maelezo anayosoma na huweza kumpa hisia fulani, kama vile, kumwacha katika hali ya taharuki. Mandhari yanayosababisha hali fulani humwezesha msomaji kujihusisha na kuelewa vyema matukio katika kazi anayoisoma. Kwa kuzisoma barua za Shaaban Robert, tunapata kuelewa haja na umuhimu wa kutilia maanani katika elimu. Suala la elimu, haswa kwa vijana, limejitokeza kuwa lenye umuhimu mkubwa sana.

Mandhari vilevile ni muhimu katika ujenzi wa wahusika na ploti ambazo hutegemea pakubwa mandhari mahsusi. Hii ni kwasababu, baadhi ya hadithi huwa na mandhari halisi ambayo huchorwa na kuelezwa, hivyo basi haziwezi kuelezwa na kutendeka katika mandhari tofauti kando na yale kusudiwa. Ujenzi wa wahusika na ploti hutegemeana pakubwa. Shaaban Robert emechora picha ya Ulenge kuwa mwanafunzi ambaye anajitahidi kusoma.

Mandhari hivyo basi ni muhimu katika *Barua za Shaaban Robert* kwa kuwa ni kipengele cha fani chenye umuhimu wa mwandishi na mhakiki. Mandhari yameonyesha uhusiano uliopo kati ya vipengele vingine vya fasihi katika mtungo huu. Katika *Barua za Shaaban Robert* mandhari yaliyotumika ni yakinifu na halisi yanayosawiri dhamira husika ya mwandishi pamoja na wahusika.

## **Hitimisho**

Makala hii imeeleza matumizi ya mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. Makala hii imejadili namna mandhari yanavyochangia katika uchoraji wa wahusika na maudhui katika *Barua za Shaaban Robert* alizomwandikia nduguye Ulenge Yusuf. Mandhari, ikiwa ni sehemu ambapo matukio ya hadithi au masimulizi hutokea huweza kumpa msanii uwezo wa kuchora wahusika na kujenga maudhui yaliyokusudiwa. Shaaban Robert katika barua zake amehusisha mila, utamaduni na historia ya Waswahili pamoja na uandishi wa barua tangu enzi za ukoloni na

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

pia umuhimu wa uandishi wa barua katika jamii. Makala hii imeonyesha kuwa Shabaan Robert aliathiriwa sana na hali ya kiuchumi na kisiasa katika uandishi wa barua hizi.

Hivyo basi *Barua za Shaaban Robert* hazipaswi kusomwa tu kama hifadhi ya kihistoria na habari kuhusu jamii ya Waswahili ya enzi ya Shabaan Robert au umaarufu wake mwandishi bali kuchukuliwa kuwa msingi wa uandishi wa nathari za Kiswahili. Barua hizi zina umuhimu wa kipekee katika taaluma na historia ya fasihi ya Kiswahili. Mbali na kutupatia taarifa kuhusu ukoo wa Shaaban Robert na Yusuf Ulenge, na kuhusu uhusiano wao wa kipekee, barua hizi zinatupa taarifa ya ziada kuhusu haiba ya Shaaban Robert, mawazo yake na namna yalivyojengeka katika ujana wake hadi uzeeni. Hapana shaka kuwa barua hizi zitatusaidia kuzielewa vizuri zaidi kazi maridhawa za Shaaban Robert, kwani zinatupa taswira nyingine isiyofahamika ya shaha huyo wa lugha ya Kiswahili.

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

### Marejeleo (References)

- Altman, J. G., (1982). *Epistolarity: Approaches to a Form*. Columbus: Ohio State University Press
- Beshukova, F.B., (2014). Media discourse of literary space in postmodernism: monograph. Maykop: AGU Publisher.
- Chatbar, S. (2006). 'Shaaban Robert: A Legend Poet and Freedom Fighter', in Daily News; Jumatano Mei, 24.
- Cook, E. H., (1996). *Epistolary Bodies: Gender and Genre in the Eighteenth-Century Republic of Letters*. Stanford: Stanford University Press.
- Donna, E. N. (1992) *The Impact of Literature-Based Reading*. Pearson Education, Upper Saddle River.
- Durant, A. n.w. (2000). *Ways of Reading: Advanced Reading Skills for Students of English Literature* (tol.2). London and New York: Routledge.
- Elistratov, V. S. (1996). Anthology of linguistic styles: on materials of the twentieth century Russian culture.(Doctor of dissertation). Moscow. 187p.
- Gakuo, J. (1996). 'Fani katika *Utenzi wa Vita vya Uhuru*'. Tasnifu ya M.Phil, Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa)
- Gibbe, A.G. (1980). *Shaaban Robert Mshairi*. Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.
- Halsband, R., (1958). 'Editing the Letters of Letter-Writers'. *Studies in Bibliography*, Juz. 11 Kr. 25-37 Bibliographical Society of the University of Virginia.
- Harries, L. (1975). "Shaaban Robert- Man of letters" *Presence Africaine* 93, 1975: 190.
- Holman, C. H. (1972) *The Roots of Southern Writing*, Athens, Georgia: Georgia University Press.
- Hutcheon, L., (1988). *The Canadian Postmodern: A Study Contemporary English-Canadian Fiction*. Toronto: Oxford University Press.
- Kezilahabi, E (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. EALB Nairobi.
- Lazar, G. (2007). *Literature and Language Teaching: A Guide for Teachers and Trainers*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Masinde, E (2012) 'Swahili Poetry and Its Forms', Nairobi.
- Mulokozi, M. M (2002) *Barua za Shaaban Robert 1931-1958*. TUKI. Dsm.
- Mulokozi, M.M. (1991). *A Survey of Kiswahili Literature: 1970-1988* Africa Focus
- Ndulute, C. (1994) *The Poetry of Shaaban Robert*. Dar-es-Salaam University Press, Dar-es-Salaam.
- Ntarangwi, M. (2014). *Uhakiki wa kazi ya fasihi*. Longhorn Publishers (K) Ltd.Nairobi.
- Perry, R., (1980). *Women, Letters, and the Novel*. New York: AMS Press.
- Sengo, T. S. Y (1973), *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake*. Longman; Dar-es-Salaam
- Shaaban Robert (1949) *Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini* Nelson, Nairobi.
- (1951) *Kusadikika*. Nairobi: Nelson.
- (1954) *Kielelezo cha insha witwatersand*, Nairobi
- (1969) *Mwafrika aimba*. Nairobi: Nelson.
- (1971) *Almasi za afrika* Nairobi: Nelson.

**Citation:** Mwavali, J. K; Nyandoro, G. O & McOnyango, O. (2020). Uchanganuzi wa Mandhari katika *Barua za Shaaban Robert*. *Journal of Popular Education in Africa*. 4(8), 42 – 55.

- (1969) *Koja la Lugha*. . Nairobi: Oxford University Press.
- (1967) *Insha na Mashairi*. Nairobi: Nelson.
- (1967) *Wasifu wa Siti binti Saad*. Nairobi: Art & Literature.
- (1968) *Ashiki Kitabu Hiki*. Nairobi: Nelson.
- (1968) *Kufikirika*. Nairobi: Oxford.
- (1968) *Pambo la Lugha*. Nairobi: Oxford.
- (1962) *Kielezo cha Fasili*. Nairobi: Nelson.
- (1959) *Masomo yenye Adili* Art & Literature, Nairobi
- (1969) *Mapenzi Bora*. Nairobi: Nelson.
- (1973) *Tenzi za Marudi Mema* na Omar Khayyam. Dar-es- Salaam: TPH.
- (1961) *Utenzi wa Vita vya Uhuru*. Nairobi: Oxford University Press.
- (1960) *Almasi za Afrika na Tafsiri ya Kiingereza*, Art & Literature, Nairobi
- (1968) *Siku ya Watenzi Wote*. Nairobi: Nelson.
- (1968) *Utubora Mkulima* . Nairobi: Nelson.
- (1971) *Mashairi ya Shaaban Robert*. Nairobi: Nelson.
- (1972) *Sanaa ya Ushairi*. Nairobi: Nelson.
- (1977) *Adili na Nduguze*. Dar-es- Salaam: TPH.
- (2002) *Barua za Shaaban Robert 1931- 1958* Dar-es- Salaam: TUKI,
- (2007) *Mithali na Mifano ya Kiswahili*. Dar-es- Salaam: TUKI,
- Sigei, Julius. (2015). ‘Shaaban Robert: Father of Kiswahili Literature’, in Daily Nation, Jumanne. Januari 6. Nairobi.
- Wafula, Richard (1989). The Use of Allegory in Shaaban Robert’s Prose Works’. MA Thesis, University of Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi. Phoenix Publishers.
- Zhukov, A. (1998). ‘Shaaban Robert in the Russian Language’ in AAP 55 kr.185-18.